

TAARIFA KWA UMMA

MAKUSANYO YA KODI KWA MWEZI WA AGOSTI 2024

Zanzibar, 03 Septemba, 2024:

1. MAKUSANYO YA AGOSTI 2024

Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), unawataarifu Walipakodi na Wananchi wote wa Zanzibar kwamba katika Mwezi wa Agosti 2024, ZRA ilikadiriwa kukusanya **Tshs. 69.490 Bilioni**, na **IMEFANIKIWA** kukusanya Jumla ya **Tshs. 71.114 Bilioni**, ambao ni **UFANISI** wa **asilimia 102.34** wa Makusanyo ya mapato yaliyotarajiwa.

Aidha, Makusanyo halisi ya mwezi Agosti ya mwaka uliopita wa 2023/2024, yalikuwa ni **Tshs 57.238 Bilioni**, ambayo yakilinganishwa na Makusanyo halisi ya Agosti ya Mwaka huu wa Fedha wa 2024/2025, yanaonesha **UKUAJI wa Makusanyo halisi wa asilimia 24.24** (Jedwali Na. 1 linatoa ufafanuzi zaidi).

Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mapato katika Mwezi wa Julai kwa mwaka 2023/2024 na 2024/2025.

Mwezi	2023/2024	2024/2025		Ufanisi (%)	Ukuaji (%)
	Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)	Makisio (Tshs. Bilioni)	Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)		
Agosti	57.238	69.490	71.114	102.34	24.24

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Zanzibar 2024

Jedwali Na. 2: Mwenendo Makusanyo ya Mapato katika Mwaka 2024/2025.

Mwezi	2023/2024	2024/2025		Ufanisi (%)	Ukuaji (%)
	Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)	Makisio (Tshs. Bilioni)	Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)		
Julai	42.897	50.490	53.322	105.61	24.30
Agosti	57.238	69.490	71.114	102.34	24.24
Jumla	100.136	119.81	124.436	103.71	24.27

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Zanzibar 2024

2. SABABU ZA KUFANYA VIZURI:

Ufikiaji wa lengo la Makusanyo ya Kodi kwa **asilimia 102.34**, pamoja na mambo mengine umesababishwa na:

- KUIMARIKA** na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, zinazotokana na sera na uongozi mzuri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zilizoimarisha mazingira ya biashara kwa pande zote mbili za Muungano.

ii. **UWEKEZAJI** mkubwa katika ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na KUIMARIKA kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

iii. **UTEKELEZAJI** wa marekebisho ya Sheria za Kodi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025. Hatua hii imepelekea KUIMARIKA kwa ukusanyaji katika vianzio vya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Ushuru wa Bidhaa, Ada za Bandari na Kodi ya Miundombinu.

iv. **KUONGEZEKA** kwa uwajibikaji wa Walipakodi katika matumizi ya Mifumo ya Ukusanyaji wa mapato wa ZIDRAS katika kulipa kodi pamoja na mfumo wa kutolea Risiti za Kielektroniki (VFMS) sambamba na kuongezeka kwa utoaji wa elimu ya Kodi kupitia njia mbali mbali.

v. **KUIMARIKA** kwa ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ya Utalii na taasisi zote za Serikali sambamba na kuimarika kwa **MAHUSIANO** na **USHIRIKIANO** kati ya ZRA na Wafanyabiashara kulikopelekea **KUONGEZEKA** kwa ulipaji kodi wa hiari .

3. MIKAKATI YA UKUSANYAJI KWA MWEZI SEPTEMBER 2024:

Katika kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi kwa Mwezi wa Septemba 2024 na miezi mengine katika Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, ZRA itaendelea kutekeleza yafuatayo:

i. **KUENDELEA kuimarisha** Kusomana (Interoperability) kwa Mfumo wa **ZIDRAS** na Walipakodi pamoja na Mifumo ya taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za Walipakodi.

ii. **KUENDELEA** kufanya ziara kwa Walipakodi ili kutambua na **KUTATUA** changamoto za Wafanyabiashara na Migogoro ya Kikodi kwa wakati, ikiwemo kuweka mazingira ya usimamizi wa sheria za kodi yatakayondoa changamoto za wafanyabiashara.

iii. **KUENDELEA** kuimarisha **MAHUSIANO** mazuri na **USHIRIKIANO** na walipakodi wote ikiwemo kusaidia kurahisisha biashara zao kisheria (Trade Facilitation) sambamba **KUIMARISHA** matumizi sahihi ya Mifumo katika usimamizi wa kodi ikiwemo KUIMARISHA elimu na Kampeni ya matumizi ya mfumo wa **RISITI ZA KIELEKTRONIKI (VFMS)**, na matumizi ya mfumo wa **ZIDRAS**.

iv. **KUENDELEZA WELEDI WA WATUMISHI** wa ZRA kwa kuwapatia mafunzo stahiki, usimamizi makini, na huduma nzuri kwa walipakodi (Customer care).

v. **KUWACHUKULIA HATUA** za Kisheria Walipakodi wachache wasiowajibika ipasavyo katika kutimiza wajibu wao wa kulipa Kodi.

4. HITIMISHO:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar inaendelea kuwashukuru Walipakodi wote kwa kuwajibika kwa HIARI katika ulipaji wa Kodi kwa Mwezi Agosti 2024. Hii ni hatua muhimu katika kutekeleza wajibu wao wa kisheria sambamba na kuchangia katika maendeleo ya Nchi.

ZRA itaendelea kuwa karibu na kuwasikiliza Walipakodi ili kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kupitia mapato hayo yatakayokusanywa kwa mashirikano ya ZRA na Walipakodi Serikali iweze kuendelea kuimarisha huduma bora za kijamii na maendeleo kwa wananchi wote.

“Tulipe Kodi Kwa Maendeleo ya Zanzibar”

Said Ali Mohamed

Said Ali Mohamed

KAIMU KAMISHNA MKUU